HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA MOROGORO KATIKA MKUTANO WA WADAU WA UTAFITI WA VIASHIRIA NA MATOKEO YA UKIMWI 2016 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MKUU WA MKOA WA MOROGORO - 24 MACHI, 2016.

Katibu Tawala wa Mkoa,
Makatibu Tawala wa Wilaya,
Wawakilishi wa TACAIDS,
Wawakilishi wa NBS,
Wawakilishi wa ICAP,
Wawakilishi wa Asasi za Kiraia,
Viongozi wa Dini,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana.

Waheshimiwa Viongozi na Wadau waalikwa, Awali ya yote ninachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo kwenye tukio hili muhimu linaloashiria ujio wa *Utafiti wa viashiria na Matokeo ya UKIMWI Tanzania wa mwaka 2016* katika mkoa wetu wa MOROGORO.

Ninakushukuruni nyote kwa kuweza kuhudhuria hafla hii licha ya taarifa ya muda mfupi na ninazishukuru taasisi zote zilizoshiriki kwenye maandalizi hadi kufikia hatau hii muhimu.

Nitumie pia nafasi hii kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Tanzania Bara na Wizara ya Afya-Zanzibar pamoja na Wadau wa Maendeleo kwa michango yao ya hali na mali na ICAP kwa kutoa ushauri wa kitaalamu katika kufanikisha utafiti huu.

Niwashukuru Viongozi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar kwa ushiriki wao katika kufanikisha maandalizi ya Utafiti huu.

Utafiti wa THIS: Utafiti wa aina hii ni wa nne kufanyika hapa nchini, unaoangalia masuala ya afya ambapo utafiti wa kwanza ulifanyika mwaka 2003/2004, wa pili ulifanyika 2007/2008 na Utafiti wa tatu ulifanyika 2011/2012.

Tafiti tatu zilizotangulia zimekuwa zikiwahusisha wananchi wenye umri wa miaka 15 hadi 49. Tofauti na tafiti hizi zilizotangulia, utafiti wa mwaka 2016 ni wa kipekee kwani kwa mara ya kwanza unahusisha wananchi wa rika zote katika kaya zilizochaguliwa.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa mara nyingine tena inafanya Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya UKIMWI ambapo pamoja na kuhusisha watu wa rika zote, lakini pia ni utafiti wa kwanza kukusanya taarifa zinazohusiana na maambukizo mapya ya VVU, kiwango cha VVU mwilini kwa watu wanaoishi na VVU na wastani wa maambukizo ya VVU kwa watu wa rika zote na wingi wa chembechembe za kinga mwilini *(CD4 T-cell count)*.

Utafiti huu utaangazia pia kuwepo kwa Viashiria vya usugu wa dawa, kiwango cha maambukizo ya kaswende na homa ya ini (Hepatitis B na C) kwa watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi. Pamoja na hayo utafiti huu utakusanya taarifa za upatikanaji na

utumiaji wa huduma zitolewazo katika kudhibiti maambukizo ya VVU na UKIMWI na Viashiria vya tabia hatarishi zinazochangia maambukizo ya VVU.

Habari njema ni kwamba utafiti wa mwaka huu utahusisha vipimo vingi zaidi ikilinganisha na tafiti za aina hii zilizopita. Aidha baadhi ya vipimo, majibu yake yatatolewa papo hapo katika kaya zitakazoshiriki.

Hali Ilivyo Kiwango cha maambukizo ya VVU katika tafiti zilizopita kinaonekana kupungua kutoka asilimia 7 mwaka 2003 mpaka asilimia 5.1 mwaka 2011. Taarifa hii inaonyesha kuwa juhudi hizo za Serikali zimeiwezesha Tanzania kupunguza kiwango cha maambukizo ya VVU kwa asilimia mbili na kuifanya Tanzania kuwa ni miongoni mwa nchi zenye kiwango cha chini cha maambukizo kati ya nchi za kusini mwa jangwa la Sahara ambapo nchini nyingi za ukanda huu zina kiwango cha maambukizo cha zaidi ya asilimia 10.

Kwa mujibu wa UNAIDS tawkimu zinaonyesha kwamba ngono zisizo salama ndiyo njia kuu ya maambukizo ya VVU miongoni mwa jamii na kina mama wakiwa na maambukizo makubwa Zaidi (53%) kuliko kina baba.

Takwimu kutoka vyanzo vingine vinaonyesha Nguvu kazi katika nchi yetu inaundwa kwa sehemu kubwa na vijana ambao ni moja ya makundi yaliyoathiriwa sana na maradhi ya UKIMWI na magonjwa mengine ya ngono kama kaswende na homa ya ini.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Wazee lipo tatizo la mimba za utotoni hapa nchini, jambo ambalo linaashiria kuwepo kwa ngono hatarishi.

Takwimu za mwaka 2012 zinaonyesha kwamba robo ya wasichana wote Tanzania wenye umri wa miaka 14 na 17 walikuwa wamejifungua angalau mara moja. Japo Mikoa inayoongoza kwa tatizo hili imetajwa kuwa ni Rukwa (asilimia 24.5) na Katavi (asilimia 27.6) lakini sote tunajua kwamba tatizo hili pia lipo kwenye mkoa wetu na linastahili kushughulikiwa.

Mahitaji ya Tawimu na Matumizi yake: Takwimu za utafiti zitawasaidia watunga sera kuandaa mikakati mipya ya kudhibiti UKIMWI inayoendana na ukubwa wa tatizo na kuimarisha mipango ya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi mbalimbali ya UKIMWI.

Aidha, takwimu hizi zitasaidia kuboresha juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali za kusogeza huduma zinazohusiana na VVU kama vile huduma za upimaji wa VVU bure kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali, kutoa huduma ya kupunguza maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) na utoaji wa dawa za kupunguza makali ya VVU zijulikanazo kama ARV.

Utafiti huu utaiwezesha Serikali kupata taarifa sahihi zitakazosaidia katika kupanga mikakati sahihi ya kuendeleza

mafanikio yanayoonekana katika mapambano dhidi ya UKIMWI ili kuokoa nguvu kazi ya taifa ambayo ni ya msingi katika kufanikisha jitihada za serikali yetu za kupambana na umaskini.

Mafanikio ya utafiti huu yatasaidia serikali kujua ukubwa wa tatizo la UKIMWI kwenye vipengele nilivyotaja hapo juu na kuisaidia serikali kuimarisha huduma husika kwa wananchi wake.

Wito Mtakubaliana nami kwamba, Sera na Mipango bora hutegemea sana upatikanaji wa takwimu sahihi na bora. Hivyo nitoe wito kwa wadau wote wa mkoa wetu kutoa ushirikiano wa Karibu kwa watafiti/Wadadisi ili kufanikisha zoezi hili muhimu kwa taifa letu.

Ninawaasa mtumie nafasi zenu kuwapokea watafiti watakapofika kwenye maeneo yanu, mfanye kila linalowezekana kuhamasisha wananchi hasa wale ambao kaya zao zimebahatika kuchaguliwa kushiriki katika Utafiti huu, waweze kutoa ushirikiano wa kutosha katika zoezi la ukusanyaji wa taarifa hizi, wakubali kufanyiwa vipimo na kupokea majibu ili waunganishwe na huduma za afya kwa wale wanaostahili. Ni vema wananchi na wadau wote wa mkoa wakaelimishwa kukubali kwamba kuijua hali ya afya ni kuijua leo na kesho ya mtu kama msingi wa kufanikisha mipango na ndoto zetu za baadaye.

Waheshimiwa viongozi na wadau wetu,

Napenda pia kuchukua fursa hii kuviomba vyombo vyote vya habari, kufikisha ujumbe sahihi kwa jamii ili kuzihimiza kaya zilizochaguliwa kutumia fursa hii adimu kujua afya zao bure bila malipo na kujiweka huru badala ya kuendelea kuishi kwa wasiwasi kwa tatizo ambalo hivi sasa linadhibitika kuliko ilivyokuwa siku za nyuma.

Kabla ya kumaliza neno langu, kwa mara nyingine tena niwasihi Wanachi wenzagu wa mkoa huu wa MOROGORO tuwe na mazoea ya kupima afya kwenye vituo vya afya ambavyo kwa sasa ni vingi ikilinganishwa na zamani, kupokea majibu ya vipimo na kujiunga katika huduma za tiba kwa wakati kwa kadiri itakavyoshauriwa na wataalamu wa afya. Kuchelewa kwenye huduma za matibabu kwa tatizo lolote la kiafya ni kupoteza fursa ya kujiongezea uhai. Ninawahimiza kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wadadisi na kuwapa taarifa sahihi zitakazosaidia Serikali na dunia kwa jumla kuwa na mango mkakati wa kuelekea kumaliza changamoto za UKIMWI ifikapo mwaka 203.Nawatakia mafanikio mema katika jukumu la kuratibu Utafiti huu.

Baada ya kusema haya, **NATAMKA KWAMBA ZOEZI LA UTAFITI WA VIASHIRIA VYA VVU/UKIMWI KWA MWAKA 2016/17 KATIKA MKOA WA MOROGORO LIMEZINDULIWA RASMI.**

WANANCHI NA WADAU WOTE TUTOE USHIRIKIANO KWA WATAFITI INDI WATAKAPOTUTEMBELEA KATIKA MAENEO YETU.

MOROGORO BILA MAAMBUKIZI MAPYA YA VVU INAWEZEKANA.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.